JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

MKOA WA DODOMA

Simu : 255 -026-2320537
Fax : 255-026-2320537
E-Mail:- ded@kongwadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 57,
KONGWA.

Kumb. Na. HW/KOG/S.20/29.VOL.IV/81 **02/03/2020**

TANGAZO LA KAZI

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira Mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa chenye Kumb. Na. FA. 170/360/01/121 cha tarehe 06 Februari, 2020 kikisomwa pamoja na chenye Kumb. Na. FA.170/360/01/96 cha tarehe 19 Septemba, 2019. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anawatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya Mtendaji wa Kijiji III kama ifuatavyo;

MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - NAFASI 7

SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe amehitimu Kidato cha Nne au sita.
- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (**NTA LEVEL 5/TECHNICIAN CERTIFICATE**) katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III:

- Kuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao.
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Kuwa katibu wa mikutano yote ya Halmashauri ya kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

Scanned by CamScanner

NGAZI YA MSHAHARA
Kwa mujibu wa Ngazi ya Mshahara wa Serikali, yaani TGS B kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI:

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi kwenye Kijiji chochote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 - 45.
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatane na Wasifu wa mwombaji (CV).
5. Maombi ya ambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha (passport size) zilizoandikwa jina la mwombaji nyuma.
6. Testimonials "Provisional Results","Results Slips", Kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA.**
7. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
8. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho *yaambatanishwe* kwenye barua ya maombi ya kazi.
9. Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa tena.
10. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 15/03/2020 saa 9.30 Alasiri.
11. Maombi yote yatumwe **kupitia posta** kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA,
S.L.P 57,
KONGWA.

LIMETOLEWA NA;
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KONGWA

Nakala: Mbao za Matangazo.
: Tovuti ya Halmashauri: www.kongwadc.go.tz
: Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma – www.ajira.go.tz

Scanned by CamScanner